# MAMBO YANAYOMFANYA MTEULE UPENDO WAKE WA KWANZA USICHUJE KWA BWANA YESU WAKE

## Maandiko EBR. 12: 1 – 3.

## 1. UTANGULIZI

Ninaposema kuchuja kwa upendo wa kwanza ninamaanisha kwamba upendo umepoteza mvuto (**unapoteza quality yake)** **( unapoteza ubora wake au sifa yake hasa**!!)

- Sote tunafahamu fika na hasa sisi tuliooa/tulioolewa kwamba siku za kwanza za kuoana, wanandoa wanafurahiana mno na wanaitana majina mazuri – mazuri; kama ni nguo wanashona za kufanana, wanatembea pamoja n.k. lakini polepole baadae wanaanza kutoana kasoro na kulaumiana na kufichana mambo yao***!!! Mwanz. 2: 21 – 25, 3: 9 – 12; 1Samwl. 18: 20 – 28, 1Samwl. 19: 11 - 17, 2Samwl. 3: 6 – 16, 2Samwl. 6: 12 - 23.***

- Sote pia tunafahamu wazi kwamba mtu kama hana ajira/kazi, moyoni mwake anakuwa anatamani afanye kazi yoyote; ngoja aipate; polepole atakapoanza kupata kipato, anaanza kukinai kazi ile na anaanza kutafuta kazi **bora zaidi** kuliko ile ya kwanza!! Hii ndiyo kawaida ya moyo wa binadamu; kufurahia sana jambo/kitu anapokipata kwa mara ya kwanza na kukichoka polepole kwa kadri siku zinavyoendelea!!! Hata iwe ni nguo au simu au gari au nyumba au kiatu n.k. mtu anavifurahia vikiwa vipya, polepole anaanza kuvichoka na kutovifurahia tena.

2. Jambo la **kwanza kabisa linaloongoza na litakalomfanya mteule upendo wake usichuje (usipoteze ubora wake) kwa Bwana Yesu ni pale atakapokuwa na tabia ya kukaa chini na kukumbuka Yesu alimkuta wapi na akamtoa huko kwa huruma zake tu. Ezek. 16:1 – 14.** Ukweli ni kwamba Mungu alilikuta Taifa la Israel likiwa katika hali mbaya sana ya utumwa huko Misri, Mungu akalitoa huko kwa mkono wake hodari na kulifanya Taifa hili kuwa la thamani machoni pake, akaliheshimu na kuwapa utukufu mwingi mbele za Mataifa mengine!! Lakini jambo la ajabu baada ya muda Israeli wakasahau hali yao ya utumwa na walikotolewa na Bwana na wakaanza kutamani kuitumikia miungu mingine!!! ***Ezek.16:15-34.*** Halafu soma hukumu itakayofuata. ***Ezek. 16:35-43.*** Dhambi inayotufanya upendo wetu uchuje mapema sana kwa Bwana wetu Yesu Kristo ndiyo hii!! ***Zek. 16: 49 –*** Pale tunapoota kiburi sababu ya shibe ya chakula na mafanikio katika maeneo mbalimbali hadi tunasahau kuwasaidia wahitaji na maskini.

3. Jambo la **pili linalomfanya mteule upendo wake usichuje (usipoteze ubora wake) kwa Bwana wake Yesu Kristo ni pale ambapo kila siku na kila saa na kila wakati anaweka macho yake kwenye furaha kuu iliyo mbele yake.** ***Ebr. 12: 1–3, Ufun. 21:1–27.*** Mitume na manabii wengi waliotutangulia pamoja na mashahidi wengi tutakaokutana nao siku moja; hii ilikuwa ni mojawapo ya siri iliyowafanya upendo wao usichuje kabisa. Wao waligundua kwamba hapa duniani hawakuwa na mji udumuo wala maisha ya kudumu!!! ***Ebr.13:14 (Ebr.11:8–10*** na hata Bwana Yesu alifundisha sana juu ya jambo hili. ***Mark. 9: 43: 50***

   - Siri ya mwanamke kuendela kuzaa ni pale anapoweka macho yake kwenye furaha ya mtoto atakayezaliwa na siyo kwenye uchungu na maumivu anayoyapitia.***Yoh.16:20 – 22.*** Siri hii ndiyo inayomfanya aendelee kuzaa hadi watoto ***4,6,8,10*** n.k.

4. Jambo la **tatu linalomfanya mteule upendo wake wa kwanza usipoteze ubora wake kwa Bwana wake Yesu Kristo (usichuje) ni pale ambapo anaepuka kabisa kumzoea Yesu na Neno lake.** ***Waam. 16: 20, Ezek. 33: 30 - 33.*** Ukizoea hata kufanya dhambi, dhambi inakuwa ni jambo la kawaida kwako na inakuwa ni vigumu kwako kuiacha!!!**Yeremia 13: 23.** Na hakuna jambo la hatari na la mtego wa hali ya juu sana na ambalo limenasa wateule wengi sana katika maeneo mbalimbali kama eneo la kuwa na mazoea na jambo Fulani!!! Leo hii tumeona ni kawaida (tumezoea) tunapoamka tu wazima tena wa afya njema!! Tumeona ni kawaida kusafiri na kurudi salama!! ***Yak. 4: 13 - 16;*** mke amemzoea mumewe na anamwona ni wa kawaida; na mume naye vivyo hivyo!!! Mazoea!!

   - Tumeona kuja kanisani na kuomba na kusikia Neno la Mungu ni jambo la kawaida tu!! **Yesu Kristo ndiye Bwana juu Mbinguni, hapa duniani na hata chini ya nchi kamwe hazoeleki/siyo wa kawaida ngo**!!!

   - **Tunapokuja mbele zake sisi ni wa kutetemeka na kuanguka chini na kusujudu na kujiona mbele zake kama wadudu wasiostahili hata kummwona uso wake!! *Isay.66:2*, Ufun. 1: 17!! Yesu ni wa kuogofya, ni wa kutetemekewa daima!! *Kut. 15:11.* Tuje mbele zake daima kwa hofu na kuogopa na kutetemeka na siyo kumzoea. Zab. 2;11 na Filip 2: 12 – 13.**

5. **Jambo la nne linalomfanya mteule upendo wake usichuje (usipoteze ubora wake) ni pale ambapo kila wakati anahesabu na kutafakari mema na mazuri ambayo Yesu amemtendea kuliko mabaya na magumu mengi anayoyapitia.** ***Filip. 4;8, Zab. 27: 1-5***

   - Iwe ni katika ndoa tu ya kibinadamu, ukiwa na tabia ya kutafakari mambo mazuri ambayo umeyapata kupitia kwa mwenzako; uzuri na ubora wa mwenzako unapanda mno mno mno. ***2Samwl. 7: 1 – 11***

   - Hata kazini, ukipata nafasi ya kukaa chini na kutafakari kwa nini wewe umeipata ile kazi wakati wengine wanaitaka lakini hawaipati, utamwona Bosi wako anayekulipa mshahara kuwa wa maana kuliko makosa anayokufanyia. **Mimi ni nani hata mtoto wa watu huyu akakubali nimwoe na akawaacha wanaume wengi, weupe, warefu, wasomi, kabila lake matajiri!!! Bwana anisaidie ili niwekeze moyo wangu kwake kama kwanza na aniondolee ile hali ya kuona vikasoro kasoro vya aina yoyote kwake; amenifanyia mambo mengi makubwa ya ajabu, amesababisha mimi kupata heshima tofauti na nilivyokuwa sijamwoa, leo naitwa Baba Mosses, Baba Mary, Baba Joshua, baba Debora!!! Leo napaka lotion!!! Leo sifugi ndevu!! Bwana nisaidie ili nisisahau ulikonikuta na ukanitoa na kunifanya hivi nilivyo leo!!! Niondolee dhambi hii ya kiburi cha uzima; dhambi hii ya kushiba chakula, dhambi hii ya kujivunia mafanikio na dhambi hii ya kuwadharau maskini na wahitaji kwa kudhania kwamba mimi nimefika hapa kwa nguvu zangu na uwezo wangu na wao wanafurahia kuwa na hali hiyo waliyo nayo. Ezek. 16: 49.**
   - **Mimi ambaye nilikuwa kama mbwa mfu tu asiye na thamani yoyote mbele za Mungu kutokana na maisha yangu ya nyuma!!! 2Samwl. 9: 1 -14. Amina**.

***Na***
***Askofu Dr. L. Mwizarubi***
***14/03/2021***